

ZIARA YA KAMATI YA SIASA YA CCM MKOA WA SONGWE



KAMATI YA SIASA CCM MKOA IMERIDHISHWA NA KUIPONGEZA HALMASHAURI YA MJI WA TUNDUMA.

Hayo yamesemwa na Mhe.Mwenyekiti kamati ya siasa CCM mkoa wa Songwe Mhe. Eneriko Mkola alipo kuwa kwenye ziara ya ukaguzi wa miradi mikubwa ya maendeleo katika Halmashauri ya Mji Tunduma.

Miradi mikubwa ya maendeleo ambayo kamati ya siasa ya mkoa iliitembelea ni mradi wa maegesho ya magari makubwa pamoja na eneo la kujenga ofisi za Halmashauri lenye ukubwa wa hekari 17, mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji Tunduma yenye hadhi ya Wilaya , ujenzi wa barabara kiwango cha lami yenye urefu wa km 0.8 pamoja na ujenzi wa vyumba sita(6) vya madarasa ya Shule ya Msingi Sogea.

Mhe. Eneriko alisema pesa zinazotumika katika miradi mbalimbali ya maendeleo zinatokana na kodi za wananchi, hivyo basi zitumike kama zilivyo kusudiwa.

Pia alisema wasimamizi wa miradi hiyo wahakikishe inakamilika katika ubora unao takiwa, ili kuhakikisha pesa za wananchi zinazo tokana na kodi zinatuma bila kuwa na ubadhilifu wa aina yoyote ile.

Vilevile alisema Ilani ya Chama Cha Mapinduzi [CCM] imejiwekea adhima ya kuwaletea wananchi maendeleo kwa ujumla. "Miradi hii itasaidia kutatua kero za wananchi pamoja na kuongeza pato la taifa."



Mhe. Eneriko Mkola aliye shika reflector jacket akiwasili katika eneo la mradi wa maegesho ya magari Halmashauri ya Mji Tunduma alipikua katika ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo mjini humo



Mhe. Eneriko Mkola akisikiliza kwa makini taarifa iliyo kua inasomwa na mhandisi wa Halmashari Dickson Kisenime katika mradi wa maegesho ya maga-

ZIARA YA KAMATI YA SIASA YA CCM MKOA WA SONGWE



Mhe. Eneriko Mkola katika ziara akikagua baadhi ya mabomba ya maji katika mradi mkubwa wa maji kata ya makambini Halmashauri ya Mji Tunduma



Maneja TBA mkoa wa Songwe Eng. Christina Gasper Shayo mbele akitoa maelezo ya mradi wa ujenzi wa hospitali ya Halmashauri ya Mji Tunduma kwa Mhe. Eneriko mloko kwenye ziara ya ukaguzi wa mradi



Baadhi ya viongozi wa chama na Serikali wakiwa katika ziara ya kamati ya siasa ya CCM mkoa wa Songwe ilipokua ikikagua miradi ya maendeleo ya Halmashauri ya Mji wa Tunduma. Wa pili kulia ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Tunduma Bi. Regina